


# MAAGIZO KUPITIA MICHORO KUHUSU HAKI ZA WAKODISHAJI VERMONT

(SWAHILI)

MICHORO YAMEUNDWA NA SOPHIE YANOW
WWW.SOPHIEYANOW.COM

MAANDISHI KUPITIA WAKODISHAJI WA VERMONT, CVOEO
CHAMPLAIN VALLEY OFFICE OF ECONOMIC OPPORTUNITY (CVOEO)

MAAGIZO HAYA YAMEUNDWA KUPITIA MSAADA WA:
BARAZA LA SANAA LA VERMONT
PAW PRINT & MAIL
MRADI WA HAKI YA NYUMBA YA CVOEO
JEAN MURRAY NA MSAADA WA KISHERIA WA VERMONT
VERMONT DEPARTMENT OF HOUSING & COMMUNITY DEVELOPMENT


NYUMBA NI HITAJI LA KIMSINGI, LAKINI SIO RAHISI WAKATI WOTE KUPATA NYUMBA NZURI, IMARA, NA KWA BEI NAFUU.G.
MAGHOROFA
HAKUNA NAFASI
KODISHA
KWA 3/4 YA MSHAHARA YAKO PEKEE $$$$
UBAGUZI UNOATENDWA KWA SABABU YA RANGI YA NGOZI, JINSIA, DINI, NA KADHALIKA, NI HATIA, LAKINI PIA UNAWEZA TENDEKA KWA NJIA ZISIZO RAHISI KUTAMBUA WAKATI UNAPOTAFUTA NYUMBA.
GHOROFA
BORA KWA WATAALAMU
CONDO
KAYA YA KIKRISTO
SICHUKUI MSAADA WA UMMA - SECTION 8.


SIDHANI MTAA HUU UTAKUFAA. WACHA NIKUONYESHE GHOROFA NYINGINE TUNAWEZA KUKODISHA.
JE, UNAONA AJE HII?
ITABIDI NIPANDISHE AMANA NA $500 KWA SABABU WATU WENU HULETA UHARIBIFU ZAIDI.
$50 ZAIDI KWA KILA MTOTO.
HATUKUBALI WANYAMA KIPENZI.

# MAKAZI YA HAKI

INI KINYUME CHA SHERIA KUBAGUA WAKATI WA KUKODISHA, KUUZA AU KUPEANA MKOPO WA KUNUNUA NYUMBA KWA AJILI YA HIZI SABABU:

JAMII YA BINADAMU
RANGI YA NGOZI
ASILI YA KITAIFA
DINI
JINSIA
HALI YA UZAZI
ULEMAVU

(HAYA YAMELINDWA NCHINI KOTE)

UMRI WA MIAKA
HALI YA NDOA
MWELEKEO WA KIJINSIA
UTAMBULISHO WA KIJINSIA
UPOKEAJI WA MSAADA WA UMMA
URAIA, HALI YA UHAMIAJI
UNYANYASAJI, KUBAKWA, KUFUATILIWA

(HAYA YAMELINDWA NCHINI VERMONT)

KAMA UNAHISI KUWA UMEBAGULIWA, PIGIA:

TUME YA HAKI ZA BINADAMU YA VERMONT
1 (800) 416-2010 AU (802) 828-2480
(SAUTI AU KIFAA CHA TTY)

MSAADA WA SHERIA YA VERMONT
1 (800) 889-2047

KITUO CHA MAISHA YA KUJITEGEMEA CHA VERMONT
(MAARIFA NA UTETEZI KWA WALEMAVU)
1 (800) 639-1522
AU (802) 229-0501
(SAUTI AU KIFAA CHA TTY)






HAKI FULANI ZIMELINDWA NA SHERIA YA VERMONT NA HAVIWEZI KUNYANGANYWA NA HATI YA KUKODISHA:

-HAKI YA KUWA NA MAKAO SALAMA NA NJEMA

-KUPEWA ILANI HALALI KABLA MWENYE NYUMBA ATEMBELEE MAKAO YAKO, APANDISHE KODI, AU AKUOMBE KUHAMA

-HAKI YA KUPINGA KUFUKUZWA KORTINI

-KURUDISHIWA AMANA YA USALAMA

LAKINI MAMBO MENGI MENGINE, HATA KAMA SI UNGWANA KWAKO, YANAWEZA TEKELEZEKA NA SHERIA BAADA YAKO YA KUTILIA SAHIHI, KAMA:

-SIKU YA MWEZI YA KULIPA KODI


-KAMA WATU WENGINE WANAWEZA ISHI NA WEWE

-WAKATI UNAPASWA KUPEANA ILANI YA KUHAMA KABLA YA KUHAMA NYUMBA


NIKI BANA KAMA TULIVYOPANGA
BAADA YA KUFANYA MAREKEBISHO MULIOKUBALIANA KWA HATI YA KUKODISHA, WEKA SAHIHI, NA...
PATA NAKALA YAKO UIWEKE MAHALI SALAMA!
HII ITAKUSAIDIA UANZISHE FAILI YENYE ITAKUSAIDIA KORTINI UKIWA NA SHIDA LOLOTE KWA MAKAZI.
KUWEKA FAILI NI NJIA MUHIMU YA KUJIKINGA KAMA MPANGAJI.
KUMBUKA JAMBO MOJA NYINGINE MUHIMU KUHUSU HATI YAKO YA KUKODISHA...
HATI YAKO YA KUKODISHA INAWEZA KOSA KUTAJA KANUNI ZA MTAA LAKINI NI JUKUMU LAKO KUZIJUA.
KWA MFANO, KAMA MTAA WAKO UNA "MASAA YA KIMYA," JIJULISHE WAKATI YANAANZA.
MASAA YA KIMYA
TAKATAKA


AMANA
AMANA NI PESA UNALIPA MWENYE NYUMBA UNAPOHAMIA NYUMBA. UNAWEZA RUDISHIWA HII PESA UKIHAMA KUTOKA HIYO NYUMBA. (HAKIKISHA ULIPEWA RISITI)
KUHAKIKISHA URUDISHIWE AMANA:
CLICK!
PIGA PICHA ZA MAKAO KABLA YA KUHAMISHA VITU VYAKO. TUNZA HIZO PICHA.
IKWA MAKAO YA BURLINGTON NA BARRE, MWENYE NYUMBA HAWEZI KUKULIPISHA ZAIDI YA AMANA YA MWEZI MMOJA (AU HATA KODI YA "MWEZI WA MWISHO") NA LAZIMA AKURUDISHIE AMANA NA RIBA YAKE UNAPOHAMA.
1 ×
AMANA INALINDA MWENYE NYUMBA KUTOKANA NA GHARAMA MPANGAJI ALIPASWA KULIPA. KWA HIVYO, MWENYE NYUMBA ANAFAA KUBAKI NA AMANA (NZIMA AU KIASI YAKE) KAMA:
-UMEHARIBU NYUMBA ZAIDI YA UHARIBIFU WA KAWAIDA
-UNA DENI YA KODI AU HUJALIPA BILI YA MATUMIZI
-MWENYE NYUMBA AMEGHARIMIKA KUTOA MALI ULIACHA KWA NYUMBA
-ULIHAMA BILA KUPA MWENYE NYUMBA TAARIFA HALALI YA KUHAMA NYUMBA


SAFISHA NYUMBA YAKO KABLA YA KUHAMA NA ONDOA MALI YAKO YOTE NA TAKATAKA. KISHA, PIGA PICHA!
CLICK
BAADA YA KUPEANA ILANI YA KUHAMA, HAKIKISHA UMEPATIA MWENYE NYUMBA ANWANI ANAFAA KUTUMA AMANA YAKO.
NAHAMIA WHITE RIVER JUNCTION.
MWENYE NYUMBA ANA SIKU 14 KUKURUDISIHIA AMANA YAKO AU ORODHA YA VITU AMETOA KUTOKA KWA AMANA NA PESA ILIYOBAKI AKULIPE.
AMANA
$800-$100=$700
ONA, HIYO ILIKUWA IMEVUNJIKA KABLA YA KUHAMIA NYUMBA.
AH, SAWA BASI.
NI LAZIMA MWENYE NYUMBA AKURUDISHIE AMANA YOTE BAADA YA HUO MUDA WA SIKU 14.
IMEKUWA SIKU 15 NA BADO SIJAPOKE AMANA YANGU
SHERIA INAHITAJI UNILIPE AMANA YOTE.
KAMA KORTI INAPATA YA KUWA MWENYE NYUMBA ALIKATAA KUKULIPA AMANA YAKO KIMAKSUDI, INAWEZA HITAJI MWENYE NYUMBA AKULIPE AMANA YAKO MARADUFU.
LIPA MDAI $1600!


FARAGHA
HODI
HODI
HODI
MWENYE NYUMBA ANAPASWA KUKUPA ILANI MASAA 48 KABLA YA KUINGIA NYUMBA YAKO, ILA YA KUTOKEA DHARURA, AU UMEMUALIKA KUINGIA.
HODI! HODI!
7:00
HODI!
ANAWEZA KUKUTEMBELEKA KATI YA MASAA YA 9AM HADI 9PM.
HABARI?
SAMAHANI, NIMEKUJA MAPEMA!
TAFADHALI RUDI 9AM.
HATA KAMA AMEKUPA ILANI, MWENYE NYUMBA ANAWEZA TU KUINGIA KWA NYUMBA BILA MWALIKO WAKO:
-KUFANYA UKAGUZI
-KUTENDA UKARABATI MUHIMU AU MLIYOKUBALIANA, MABORESHO AU HUDUMA FULANI
-KUONYESHA NYUMBA KWA WAPANGAJI WATARAJIWA, WANUNUZI, AU WAFANYAKAZI
WAPANGAJI HAWAWEZI NYIMA MWENYE NYUMBA RUHUSA YA KUINGIA BILA SABAU HALALI.
BASI ITABIDI NIWACHE KULIPIA JOTO YA NYUMBA



KODI
HAKIKISHA UMELIPA KODI YA NYUMBA KWA KUTUMIA CHEKI AU ITISHA RISITI UNAPOLIPA NA FEDHA TASLIMU.
HII INAKUSAIDIA KUWEKA REKODI YA VILE UMELIPA KODI YA NYUMBA KWA WAKATI UNAOFAA.
ONGEZEKO LA KODI YA NYUMBA
NINAONGEZA KODI KATIKA WIKI MBILI.
UNA HAKI YA KUPEWA ILANI YA SIKU 60 KABLA YA KUONGEZESHWA KODI YA NYUMBA (SIKU 90 UKIWA BURLINGTON)
UNAHITAJIKA KUNIPA ILANI ZAIDI YA HIYO.
MWENYE NYUMBA HAWEZI ONGEZA KODI YA NYUMBA WAKATI WA UKODISHAJI WAKO, ILA KUWA IMENENWA KWA HATI YA KUKODISHA.
HATA MIMI NIMELINDWA NA HATI YETU YA KUKODISHA.
KUPUNGUZA HUDUMA (KAMA KUTOA JOTO YA NYUMBA, TAKATAKA, KUTOA THELUJI, NA KADHALIKA), YOTE YAHUSIKANA NA KUONGEZA KODI YA NYUMBA
BASI ITABIDI NIWACHE KULIPIA JOTO YA NYUMBA.
HATA HIYO INAHITAJI ILANI ZAIDI.

# MAKAZI MEMA


WAPANGAJI WOTE WANA HAKI YA MAKAZI SALAMA NA MEMA. HAUWEZI POROSHWA HAKI HIYO KWENYE HATI YA KUKODISHA.

MIFANO NI KAMA:

USALAMA WA MOTO: KUTOWEZA KUTOROKA KUPITIA MADIRISHA YA VYUMBA VYA KULALA, KUTOKUWA NA VICHUNGUZI VYA MOSHI NA KABONI MONOKSIDI.



MAJI YA BOMBA YA KUNYWA, MAJI MOTO, VYOO VINAVYOFANYA KAZI, BESHENI JIKONI, BAFU, NA NJIA YA KUTOA MAJI TAKA



MIUNDO SALAMA, YAKIWA NA MILANGO, DIRISHA ZINAZOFUNGA, NA PAA ZISIZOVUJA




MIFUMO YA JOTO YANAYOWEZA LETA JOTO ANGALAU 65F (18C) KATIKA MIEZI BARIDI



NYUMBA ILIYO SALAMA KUTOKA MADHARA YA SUMU RISASI, YENYE INADHURU HASWA BONGO ZA WATOTO WACHANGA. WATOTO WANAWEZA PUMUA VUMBI YA SUMU YA RANGI INAYOPOROMOKA.




NYUMBA ZILIZOJENGWA KABLA YA 1978 ZILIPAKWA RANGI YA SUMU RISASI.
1872 CENTENNIAL HOUSE
WENYE NYUMBA WA MAKAO YALIYOJENGWA KABLA YA HUO MWAKA WANAFAA KUFANYA MATENGENEZO KILA MWAKA ILI KUHAKIKISHA RANGI HAIPOROMOKI AU HAITOKANI.
MWENYE NYUMBA YAKO ANAPASWA KUHAKIKISA UNA MAKAO SALAMA YA KUISHI.
NI WAJIBU WAKO KULINDA NYUMBA NA KUJULISHA MWENYE NYUMBA UNAPOONA NYUMBA INAHITAJI UKARABATI.
HII NI MUHIMU KWA USALAMA WAKO NA KUHAKIKISHA UTARUDISHIWA AMANA YAKO UKIHAMA.
UKIFANYA UHARIBIFU, MWENYE NYUMBA ANAWEZA KUKUGHARIMU MATENGENEZO, LAKINI NI YEYE NDIYE ANAPASWA KUFANYA HAYO MATENGENEZO.


MATENGENEZO
OFISI YA POSTA
KAMA MWENYE NYUMBA HATATENDA MATENGENEZO, MUOMBE KWA BARUA.
HI INAKUWA REKODI YA MAANDISHI YA VILE ULIAMBIA MWENYE NYUMBA JUU YA MATENGENEZO, NA INAKUSAIDIA KUPATA MSAADA WA SHERIA.
WEKA NAKALA
KAMA INALETA MADHARA YA USALAMA AU AFYA, PIGIA AFISA WA AFYA WA MTAA AU KITENGO CHA USALAMA WA MOTO CHA VERMONT.
NAFIKIRI JOTO YA NYUMBA IMEHARIBIKA NA MWENYE NYUMBA HAJI!
WASILIANA NA VT TENANTS IKIWA UNAHITAJI USAIDIZI WA KUAMUA NI NANI UTAMPIGIA SIMU.
WATAKUJA KUFANYA UKAGUZI NA WANAWEZA TOA ILANI KWA MWENYE NYUMBA KUSULUHISHA HIYO SHIDA.
NI VYEMA ULITUPIGIA.
NITAWASILIANA NA MWENYE NYUMBA
UNALINDWA NA SHERIA IKIWA MWENYE NYUMBA ATAJARIBU KUKUFUKUZA, KUPANDISHA KODI YA NYUMBA, AU KUKUNYANYASA KWA NJIA LOLOTE KWA SABABU ULIPIGIA INSPEKTA.
WEKA NAKALA YA RIPOTI YA INSPEKTA. UNA HAKI YA KUPEWA HIYO NAKALA NA NI MUHIMU KUIWEKA KWA FAILI ZAKO.
RIPOTI


KAMA MWENYE NYUMBA HATAFANYA MATENGENEZO YANAYOHITAJIKA KWA MUDA MWEMA, UNA HAKI YA...
KUVUNJA HATI YA KUKODISHA NA KUHAMA
KUSHTAKI MWENYE NYUMBA KORTINI ILI ULIPWE FIDIA
UREKEBISHE HIYO SHIDA WEWE MWENYEWE NA UTOE GHARAMA KUTOKA KWA KODI YAKO YA NYUMBA
...AU USILIPE KODI YA NYUMBA HADI ITATULIWE.
SIWEZI LIPA HADI UREKEBISHE JOTO YA NYUMBA.
KILA MOJA YA SULUHISHO HIZI INAPATIKANA TU KATIKA HALI FULANI, KWA HIVYO PIGIA VERMONT TENANTS KABLA UZIJARIBU.
VT TENANTS
802-864-0099 OR
1-800-287-7971
VTTENANTS.ORG

# KUHAMA

UNAPASWA KUPATA ILANI YA MAANDISHI YA SIKU 14-120 MWENYE NYUMBA ANAPOTAKA UHAME..

DKULINGANA NA SABABU, PAHALI UNAPOISHI, NA MUDA ULIPOISHI KWA HIYO GOROFA. TUPIGIE ILI TUKUSAIDIE NA KESI YAKO.

NI LAZIMA UPEANE ILANI KABLA YA KUHAMA: ANGALAU KIPINDI MOJA CHA KUKODISHA (MBILI UKIWA BURLINGTON), ILA IKIWA HATI YAKO YA KUKODISHA INAPEANA KIPINDI TOFAUTI.




UKIAMUA KUHAMA MAPEMA, INAWEZA BIDI ULIPE KODI YA NYUMBA HADI MUDA WA KUKODISHA KULINGANA NA HATI IISHE AU MKODISHAJI MWINGINE AICHUKKUE.




UNAPOHAMA, UNASTAHILI KUONDOA MALI YAKO YOTE NA TAKATAKA, NA UWACHE NYUMBA IKIWA SAFI ILI URUDISHIWE AMANA.



CHUKUA PICHA ZA NYUMBA BAADA YA KUHAMA ILI UWE NA REKODI YA HALI YA NYUMBA ULIVYOIWACHA!



USISAHAU KUPATIA MWENYE NYUMBA ANWANI YA KUKUTUMIA AMANA.



# KUFUKUZWA


ILANI ILIYOANDIKWA YA KUMALIZA UKODISHAJI NDIO HATUA YA KWANZA YA KISHERIA YA KUKUFUKUZA.




KAMA UNAAMINI YA KWAMBA UNAITISHWA KUHAMA KWA NJIA ISIYO HALALI KAMA KWA AJILI KUBAGULIWA, KULIPIZA KISASI KWA SABABU ULIOMBA MATENGENEZO, AU KAMA HUJAPEWA ILANI HALALI, UNAWEZA KUPINGA OMBI LA KUHAMA..





KATIKA KESI HII, MWENYE NYUMBA LAZIMA AKUPELEKE KORTINI KATIKA MCHAKATO RASMI WA KUFUKUZWA.



KUFUKUZWA NYUMBANI NI MCHAKATO MAALUM WA KORTI, NA MWISHOWE JAJI HUFANYA UAMUZI WA MWISHO.




NI KINYUME YA SHERIA MWENYE NYUMBA KUKUFUKUZA KWA NJIA YA KUZIMA HUDUMA, KUBADILISHA VIFULI, KUTUPA MALI YAKO, AU KUZIBA UWEZO WAKO WA KUTUMIA MAKAO.




KUFUKUZWA NYUMBANI INAWEZA KUWA BEI GHALI, NA SIFA MBAYA KUTOKA MWENYE NYUMBA INAWEZA KUZUIA KUKODISHA NYUMBA NYINGINE. HAKIKISHA UNA KESI MULWA KABLA YA KUENDA KORTINI.




PIGIA MWANASHERIA UKIWAHI PATA ILANI YA KUHAMA! NAMBARI YA USAIDIZI WA SHERIA NI 1-800-889-2047.

# RASILIMALI

## NAMBARI ZA SIMU ZA USAIDIZI KWA WAKODISHAJI:

VT TENANTS (802) 864-0099 AU BILA MALIPO 1-800-287-7971
VTTENANTS.ORG

USAIDIZI WA SHERIA ZA VERMONT 1-800-889-2047
VTLAWHELP.COM

## FAIR HOUSING COMPLAINT LINE:

VERMONT HUMAN RIGHTS COMMISSION
1-800-416-2010 OR (802) 828-2480 (VOICE/TTY)
HRC.VERMONT.GOV/HOW-TO-FILE

## NAMBARI YA MALALAMIKO YA NYUMBA YA HAKI:

TUME YA HAKI ZA BINADAMU YA VERMONT 1-800-416-2010 AU (802) 828-2480 (USAIDIZI KWA SAUTI/TTY)
HRC.VERMONT.GOV/HOW-TO-FILE

## MAFUNZO YA VIKUNDI YA NYUMBA YA HAKI:

CVOEO FAIR HOUSING PROJECT
802-660-3455 UGANI 106
CVOEO.ORG/FHP

## SHERIA NA KANUNI ZINAZOHUSIANA:

KANUNI ZA JIMBO LA VERMONT: KICHWA 9: BIASHARA NA SOKO
SURA 137: MAKUBALIANO YA KUKODISHA MAKAZI
LEGISLATURE.VERMONT.GOV/STATUTES/CHAPTER/09/137

KANUNI ZA VERMONT ZA AFYA KWA MAKAZI
WWW.HEALTHVERMONT.GOV/REGS/RENTAL_HOUSING_CODE.PDF

KANUNI ZA MOTO NA USALAMA WA MIJENGO
FIRESAFETY.VERMONT.GOV

cvoeo

Champlain Valley Office of Economic Opportunity

cvoeo.org